# NAMBA 7: MARKO 11:1-11 MFALME ALIYEPANDA PUNDA!

Mnamo tarehe **nne** Desemba miaka elfu moja, mia tisa na sabini na saba, umati ulikusanyika katika nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati, kushuhudia mtu aliyekuwa akiapishwa kuwa Rais wa nchi yake. Jina lake lilikuwa **Jean Bedel Bokassa**. Alikuwa amejitangaza mwenyewe kuwa Rais wa nchi yake milele! Alikuwa amejitangaza kwamba yeye mwenyewe angekuwa Waziri Mkuu. Alikuwa amejiinua yeye mwenyewe kuwa 'mkuu' katika jeshi, na pia alitangaza kwamba, atakuwa kiongozi wa chama cha kisiasa cha nchi. Kulikuwa na chama kimoja tu cha kisiasa. Alikuwa ameivunja Katiba iliyokuwepo, na katika sherehe hii kuanza utawala wake, alijipatia mwenyewe jina hili: '*Utawala wake wa Kifalme wa Jamhuri ya Afrika ya Kati'*. **Bokassa** alijaribu kuhala-lisha vitendo vyake, kwa kusema kwamba kama angejiita mfalme, angeisaidia nchi hiyo kutambulika katika maeneo mengine ya bara. Alitumia zaidi ya dola **milioni kumi na tatu** katika sherehe hiyo tu, ambayo ni robo **tatu** ya bajeti ya kila mwaka ya nchi!

Asubuhi ya siku ya sherehe hizo, wakati umati ulipokusanyika kwenye uwanja huo, ngoma hizo zilikuwa zilikuwa zikipigwa, na baragumu zilikuwa zikichezwa. Muziki ulikuwa wa sauti kubwa! Sherehe hizo zilianza kwa watoto **wanane** wa Bokassa, walipoingia wakitembea kwa mstari, katika zulia la kifalme kuelekea kwenye viti vyao. Kwa jumla alikuwa na watoto wapatao **ishirini na tisa**! Alikuwa na wake **tisa**, na mke wake kipenzi aliitwa Catherine, ambaye alikaa karibu naye. Catherine alikuwa amevaa mavazi yaliyotolewa katika nchi ya Ufaransa, ambayo yalikuwa na thamani zaidi ya dola **elfu arobiani na sita**! Bokassa mwenyewe, aliwasili katika sherehe hizo akiwa katika gari iliyotengenezwa kwa dhahabu, gari hiyo ilikuwa inavutwa na farasi **sita.** Bokassa alikuwa amevaa joho lililokuwa limepambwa kwa maelfu ya lulu. Bokassa aliketi kwenye kiti cha enzi, ambacho kilikuwa kimetengenezwa katika umbo la tai mkubwa, na wakati sherehe zikielekea mwisho, alijivika taji la dhahabu kichwani pake, ambalo lilikuwa na thamani ya zaidi ya dola milioni moja. Umati wa watu ulishangilia, na kupunga mikono. Jeshi lilisimama kwa umakini alipokuwa anavikwa taji ya kuwa mfalme wa Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Kwa miaka kadhaa, bara la Afrika limeshuhudia mifano mingi ya viongozi, ambao walikuwa na njaa sana ya madaraka. Walikuwa na tamaa ya kuwa Maraisi wa nchi zao. Baadhi yao walikuwa watu wa kiimla, ambao walinyeshwa sumu na madaraka. Waliharibika, na kusababisha uharibifu mkubwa kwa nchi zao. Jean Bedel Bokassa alikuwa mmoja wa watu hawa. Alitawala kwa **miaka kumi na nne**, na alisababisha mateso mengi na makubwa kwa watu wa nchi yake.

Hatimaye aliondolewa kutoka madarakani, na kukamatwa kwa ajili ya ufisadi wake, na aliwekwa gerezani. Cha kusikitisha, viongozi wengi wana hamu ya kuinuliwa juu zaidi ya wengine. Wanatamani kuangaliwa kama watu, ambao ni wa muhimu sana. Wanapenda kufikiria kuwa wana uwezo wa kufanya chochote kile wanachokitaka, bila ya uwaji-bikaji wowote. Hiyo ni ishara ya kiongozi mbaya.

Basi, katika kipindi hiki, tunakwenda kumwangalia kiongozi tofauti sana, na uwekwaji wa tofauti sana wa ufalme mpya; akiingia kwa furaha na ushindi **Yerusalemu**, kwa mfalme wa Israeli. Hii ilikuwa ni habari tofauti sana, na habari ya Jean Bedel Bokassa. Hii ni habari ya mtu ambaye alikuja kutumika, na si kwa kutumikiwa. Huyu alikuwa ni mtu ambaye alikuja katika unyenyekevu, ingawa alikuwa ni Mwana wa Mungu. Kwa kweli, kuna mstari mmoja katika **Zekaria sura ya tisa** unaoonyesha ni jinsi gani sherehe hii ilivyo ya tofauti. Zekaria

alikuwa nabii aliyeishi katika Israeli **miaka mia tano** kabla Yesu kuzaliwa – lakini aliandika kuhusu kuingia kwa ushindi kwa Yesu. **Zekaria sura ya tisa, mstari wa tisa** inasema hivi: "*watu wa Yerusalemu; tazama, mfalme wenu anakaribia; Yeye yuaja kwenu; Yeye ni mnyenyekevu na mpole, na anakuja amempanda punda, hata juu ya mwana punda*". Ni tofauti kubwa sana! Nafikiri tunahitaji kusoma hadithi hii katika Marko, sura ya kumi na moja, mstari wa kwanza hadi kumi na moja.

Katika siku ya Jumapili ya kwanza ya mitende katika Yerusalemu, Je, unaweza kufikiria jinsi ilivyokuwa? Afisa wa Kirumi, akiendesha farasi, kwenda kuona kinachoendelea kwenye **Mlima wa Mizeituni**. Alikuwa ameuona umati ule wa watu ukiwa umekusanyika pamoja juu ya kilima. Na hivyo alitaka kuangalia kile kinachotokea. Na kisha anaona maandamano ya watu wakishuka chini ya mlima. Siyo maandamano kama yale ambayo alikuwa amehudhuria huko **Roma**. Yeye alikuwa amezoea kuona maandamano makubwa - lakini haya yalikuwa ni ya tofauti. Alipoyaangalia maandamano haya kwa ukaribu, anaona kwamba wengi katika umati ule ni watu maskini na watoto. Wengi wao ni wakulima kutoka Galilaya na Bethania. Wanapiga  makofi, na kuimba, na wakipunga matawi ya mitende. Na afisa anapomwangalia mtu aliyeongoza maandamano haya, hakumwona mfalme katika gari, bali anamwona mtu aliyempanda mwana punda, akiwa na koti la kuazima limetandazwa mgongoni mwa punda. Haya yalikuwa maandamano tofauti sana, na yale ya kifalme huko Roma. Wakati mwingine tunaposoma magazeti, au kutazama televisheni, tunaona picha za Raisi akihutubia umati wa watu mitaani, au katika uwanja. Umati wa watu hukusanyika; wanaimba, na kupiga makofi, wakati ambapo Raisi unapowasili.

Rais Magufuli anapofika, anatoka nje ya gari lake, anashikana mikono na watu wengi, na kisha anatembea kwenda kwenye jukwaa ambapo anaanza kuzungumza. Hicho ndicho hutokea. Lakini fikiria jinsi ambavyo ingekuwa kama Rais angeliamua kufanya mambo tofauti. Badala ya gari, yeye angewasili akiwa juu ya punda! Mtu muhimu zaidi katika nchi, kufika akiwa juu ya punda! Ni kamwe kutokea - lakini hayo ndiyo yanachotokea hapa katika injili ya Marko, na huyu si mfalme wa kawaida; ni **Mfalme wa Israeli**. Ni Mwana wa Mungu; Wafalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana; ni Muumbaji wa ulimwengu wote - na hapa yeye alikuwa akiuingia mji, akiwa juu ya mwana punda! Ni picha ya ajabu ya unyenyekevu, na upole. Ni picha ya mtu ambaye alikuja kutumika, na si kutumikiwa; picha ya mfalme ambaye anakuja kama mtumishi.

Je, nini hasa kinachotokea hapa katika Marko **sura ya kumi na moja**? **Mstari wa kwanza** unatuambia kuwa Yesu na wanafunzi wake walikuwa wanakaribia Yerusalemu na vijiji vya Bethfage na Bethania. Walikuwa wametembea kutoka mji wa Yeriko, mwendo wa kilometa **ishirini na tano** hivi. Yesu alikuwa amemponya tu mtu kipofu aitwaye **Bartimayo**. Hatujui mengi kuhusu Bethfage – ilikuwa kijiji kidogo kwenye mlima wa mizeituni. Kwa kweli, kimetajwa mara moja tu katika Biblia hapa katika Marko sura ya **kumi na moja**. Tunajua habari kidogo zaidi kuhusu Bethania; kilikuwa ni kijiji, kilichokuwa pia juu ya mlima wa Mizeituni, na Injili ya **Yohana sura ya kumi na moja** inatuambia kwamba Yesu alikuwa na marafiki ulioishi huko; Mariamu, Martha, na Lazaro. Inaonekana kutoka katika maandiko kwamba, mara nyingi Yesu alitumia muda kadhaa huko. Kwa kweli, katika injili ya Yohana, habari ya Lazaro kufufuliwa kutoka kwa wafu, ilikuja wiki moja kabla ya kuingia kwa furaha na ushindi.

Walipokuwa wanavikaribia vijiji hivi, Yesu anawageukia wanafunzi wake, na kisha aliwaomba wawili wao waendelee mbele; akiwaelekeza kwenda kuleta mwana punda mdogo ambaye

wangemkuta amefungwa mbele ya mlango wa nyumba ya mtu mmoja. Je, Yesu aliwezaje kujua punda huyu alikuwa pale? Hatujui - Biblia haituambii. Labda mmoja wa wanafunzi wake alikuwa amemwambia; labda aliwajua watu katika kijiji hicho ambao wanalimiliki punda, au labda alifunuliwa na Mungu Baba. Hatujui, lakini kile tunachokijua ni kwamba haya yote yalikuwa yamepangwa na Yesu. Alikuwa amepangilia kila kitu. Katika **mstari wa nne** tunaona kwamba wale wanafunzi wawili walienda, na walimpata punda mahali pale pale, ambapo Yesu alikuwa amesema angekuwa. Yesu alikuwa amejiandaa kuwa kuna uwezekano kwamba mtu angewauliza swali juu ya matendo yao. Mistari ya **tano na sita** inasema:

"*Baadhi ya watu waliokuwa wamesimama pale, waliuliza ni kwa nini walikuwa wanamfungua punda, na wale wanafunzi wawili walijibu kama Yesu alikuwa amekwisha-waambia kufanya - na hivyo watu wale waliwaacha waende zao*". Sijui ni kitu gani wanafunzi walikuwa wanakifikiria, walipokuwa wakienda kwenye kijiji kile, ili kumfuatilia na kumleta punda huyu, lakini walionekana kana kwamba walikuwa wanamwiba punda huyu! Lakini wanafunzi hawa hawakumhoji Yesu – wao walitii tu na kwenda kwenye kijiji katika utii mkamilifu. Angalia katika **mstari wa pili**. Yesu alisema "**Enendeni**" na **mstari wa nne** unaonyesha kwamba walienda.

Ninapoyasoma hayo, huwa kuna swali ambalo ninalotaka kuuliza hapa ni hili: Je, ninaishi maisha yangu yenye utiifu kamili wa Kristo? Niko tayari kumtii Mungu wakati anaponiomba kufanya kitu kwa ajili yake? Au ninataka kubishana naye juu hicho anachoniagiza? Huenda Mungu amekuwa akikuomba ufanye kitu kwa ajili yake. Kwa kweli, maelekezo yake yamekuwa wazi sana – lakini umechagua kutomtii. Badala yake, umechagua kukaa 'nje ya kijiji', badala ya kutembea katika mwelekeo, ambao Mungu amekusihi kwenda. Kama wewe ni Mkristo, Yesu anauomba utii wako kamili.

**Mstari wa saba** unasema kwamba walimleta mwana punda kwa Yesu; waliweka mavazi yao juu yake, na Yesu akaketi juu yake - na kisha waliendelea kwenda katika barabara na mitaa ya Bethania, na walishukia chini ya **Mlima wa Mizeituni**, katika kuingia Yerusalemu Umati wa watu walikuwa wamesimama karibu na barabara, wakishangilia na kuimba wakati alipokuwa akipita. Mji wa Yerusalemu ulikuwa mahali pa shughuli nyingi sana wakati huu wa mwaka, kwa sababu Pasaka ilikuwa karibu kuanza. Mitaa ilikuwa imejaa watu, na wengi wa watu hawa walikuwa wamesikia juu ya habari za Yesu; walikuwa wamesikia kuhusu mtu ambaye alikuwa akifanya miujiza, na hata kuzungumza kinyume ya viongozi wa Kiyahudi. Katika mji huu kulikuwa na wasiwasi mwingi, kwa sababu viongozi wa Kiyahudi walikuwa na wivu dhidi ya umaarufu wa Yesu. Kwa siri siri walikuwa wanapanga kumwua.

Sasa, hadi wakati huu katika huduma yake, wakati wowote watu walipoanza kusema kwamba Yesu alikuwa ni Masihi, Yesu alitoka katika maisha ya hadhara ya watu, na kwenda mahali mbali na umati, kwa sababu alitaka kuepuka umaarufu wa hadharani. Alikuwa hata akiwaambia wanafunzi wake wasiwaambie watu kwamba yeye alikuwa ni Masihi - lakini sasa katika Marko sura ya **kumi na moja**, ni tofauti kabisa. Hapa tunamwona alikuwa amempanda punda akiingia Yerusalemu - na kipindi hiki, alikuwa akiwaruhusu umati wa watu kuimba sifa zake; alikuwa akiwaruhusu kumuimba yeye kuwa ni Masihi. Kwa kweli, katika injili ya **Luka**, Mafarisayo walimwambia Yesu awaambie wanafunzi wake wanyamaze kimya.

Hawakutaka kusikia kwamba Yesu alikuwa ni Masihi. "*Waambie wanafunzi wako, na uwaambie umati uache kupiga kelele kwamba wewe ni Masihi*". Je, majibu ya Yesu ni yapi? Luka anatuambia juu ya kile ambacho Yesu alisema (Luka 19:40): "*kama watanyamaza kimya, hata mawe yatapiga kelele; yangeweza kupiga kelele kwamba mimi ni Masihi*"! Hivyo, ni wazi kwamba kwa sasa Yesu anaukaribisha umma umtambue yeye kama Masihi. Kwa nini? Kwa sababu ulikuwa ni muda sahihi. Lakini kwa nini Yesu alichagua kuuingia mji akiwa amepanda juu ya punda? Hiki killikuwa ni kipindi ambacho Yesu alikuwa akitangaza kuwa Masihi – kwa hiyo, kwa nini hakutaka kuuingia mji akiwa katika gari kubwa, au hata kwenye farasi mkubwa? Badala yake, Yesu anachagua punda mdogo! Kwa nini? Tayari nimeshautaja mstari huu – lakini Yesu anataka kutimiza unabii ambao ulikuwa umetolewa juu yake miaka **mia tano** iliyopita. **Zekaria sura ya tisa, mstari wa tisa**: *"Furahini sana, Ee binti Sayuni! Piga kelele, binti Yerusalemu! Tazama mfalme wako anakuja kwenu, mwenye haki na wokovu, mpole na amempanda punda, juu ya mwana-punda*". Na hapa – Yesu anatimiza unabii huo. Yesu anawataka watu wajue kwamba yeye ni Masihi aliye-ahidiwa.

Katika injili ya **Luka** tunaambiwa kwamba Yesu alimchagua punda, ambaye hakuna mtu aliyewahi kumpanda kabla (Luka 19:30). Na hata katika maelezo haya madogo, kuna madhumuni. Kulingana na Agano la Kale, mnyama ambaye alijitenga kwa ajili ya kazi takatifu, ilibidi awe mnyama ambaye hakutumiwa kwa madhumuni ya kawaida. Fikiri juu ya hilo. Hapa palikuwa punda huyu mdogo, ambaye alikuwa hajapandwa kabla - na sasa, yu tayari kumbeba abiria yake Mtakatifu kushuka Mlima wa Mizeituni, na katika mitaa ya Yerusalemu. Huyu ndiye Mfalme wa Amani, akiingia mjini. Angalia katika **Mstari wa nane** - tunaambiwa kwamba wakati maandamano hayo yakiingia Yerusalemu, watu wengi waliziweka nguo zao chini ardhini, kama ishara ya heshima. Hii ilikuwa ni ishara kwamba watu hawa walimtambua kwamba Yesu alikuwa mfalme wao. Walikuwa wakimruhusu atembee juu ya nguo zao. Walikuwa wakisema, "*huyu hapa ni mfalme. Mimi naweka nguo yangu mbele yake na anaweza kuzikanyaga. Mimi nayatoa maisha yangu kwake*". Watu wengine walikuwa wakikata matawi kutoka kwenye miti. Yohana, katika injili yake, unatuambia kuwa walikuwa na matawi ya mitende, na waliyaweka chini kwenye barabara ya vumbi, ili kwamba Yesu aweze kutembea juu ya zulia!

Wengine walikuwa wakipiga makelele na kuimba. **Mistari ya tisa & kumi** inatuambia kwamba - "*wale ambao walienda mbele, na wale waliowafuata, walipiga kelele 'Hosana – ubarikiwe ufalme ujao wa Baba yetu Daudi. Hosana mbinguni juu"*. Watu walikuwa wakimsifu Yesu – walikuwa wakipata msisimko kwamba Masihi wao alikuwa amekuja. Vipi kuhusu neno '**Hosana**'? Hili lilikuwa ni neno ambalo ilitumika kama salamu ya kidini katika sherehe ya Pasaka. Kilikuwa ni kilio cha matarajio ambacho kilimaanisha '*okoa*' au '*tuokoe*'. Na watu walikuwa wakiimba neno hili tena na tena: Hosana! Tuokoe! Tuokoe! Ni kutangaza kwamba Yesu alikuwa Mwokozi wao; Mkombozi wao; alikuwa anakaribishwa kama mtu ambaye angewaokoa kutoka kwa Warumi - hivyo ndivyo walivyofikiri. '*Amebarikiwa yule ambaye anakuja katika jina la Bwana'*.

Yesu alikuwa akiwaambia watu kwamba alikuwa amekuja kwa jina la Bwana; na ya kwamba yeye alikuwa ametumwa kwao na Mwenyezi Mungu. Na sasa anawaambia, "*ninakuja kwako kama Mwana wa Mungu, na ninakuja kwa mamlaka ya Mwenyezi Mungu*". Huyu ni Mwana wa Mungu, na alikuja ulimwenguni ili kuwaokoa wenye dhambi, na kuleta uhuru kwa watu – si uhuru kutoka kwa Warumi, bali kutoka katika utumwa wa dhambi zao. Kwa kweli, kitabu cha **Matendo ya Mitume sura ya nne, mstari wa kumi na mbili** inasema haya: *"wokovu haupatikani kwa mtu mwingine yeyote, kwani hakuna jina lingine chini ya mbingu tulilopewa*

*wanadamu kuokolewa kwalo".* Ni nani awezaye kutuokoa kutoka kwenye dhambi zetu? Je, ni Allah? Je, ni Buddha? Ni nani? Ni Yesu pekee ambaye anaweza kutuokoa kutoka kwenye dhambi zetu. Ni yeye pekee tunayepaswa kumsifu, kwa kuwa ni yeye peke yake aliyetuokoa.

Tunapokaribia kufika mwisho, ngoja nitaje mstari mmoja katika **Yohana sura ya kumi na mbili - mstari wa kumi na sita**. Unatuambia kwamba, wakati fulani katika maandamano, wakati wanafunzi walikuwa wakiuangalia umati wa watu; waliposikia yale watu walikuwa wanayaimba: "*hawayakuelewa yote ambayo yalikuwa yanaendelea".* Ingawa walikuwa na Yesu kwa miaka **mitatu** hawakuelewa kile kilichokuwa kikitendeka. Nadhani walikuwa bado wanatarajia Masihi Mfalme ambaye angepigana dhidi ya majeshi ya Kirumi, na kuwafukuza kutoka katika nchi yao ya ahadi. Wakati ule walipokuwa wanamwangalia Yesu akiwa amempanda mwana punda, katika akiwa anauingia mji - nina hakika kwamba baadhi yao walikuwa wamekata tamaa kwamba Yesu hakuwa shujaa aliyekuwa tayari kwa ajili ya vita. Walimtaka yeye apigane na Warumi, lakini hapa tunamwona akiwa amempanda mwana punda. Sidhani kama Afisa huyu wa Kirumi alikielewa kile kilichokuwa kinaendelea. Inawezekanaje mtu huyu kuwa mfalme? Mafarisayo na Walimu wa sheria hawakuelewa. Je, ni kwa namna gani mtu huyu mpole na wa amani, anaweza kweli kuwa Masihi aliyeahidiwa? Walikuwa na picha tofauti sana, ya vile walivyotaka mfalme wao kuwa. Hata wengi wa wale kwenye umati, ambao walikuwa wakimsifu kama Mwokozi wao, walikuwa hawaelewi kwa kweli kile walichokuwa wanakiimba. Wiki moja baadaye, wengi wao walikuwa tayari wameshaamua kwamba hakuweza kweli kuwa Masihi; wengi wa hawa watu walikuwa wakipiga kelele asulubiwe. Na hata leo, watu wengi katika jamii yetu hawawezi kuelewa madai ya Kristo. Hawawezi kuona ni kwa jinsi gani Yesu anaweza kuwasaidia, na kuwakomboa kutokana katika dhambi zao. Na hao ni vipofu wa kweli. Mioyo yao ni migumu sana. Na hawaamini kwamba mtu yule ambaye alimpanda punda, anaweza kuwa mfalme wa maisha yao. Angalia **mstari wa tisa** tena – kazi yetu ni nini? Kama mchungaji au mwinjilisti, kazi yako ni nini? *"Ni wale walioendelea mbele, na wale waliofuata wakipiga kelele 'Hosana".* Tunapaswa kuwa kama watu wale wa kwenye umati. Kazi yetu ni kuwaambia watu wengine kwamba Yesu ni Mfalme.

Tunapaswa kuwaambia wale walio kanisani, na wale walio nje ya Kanisa, kwamba Yesu ni Bwana, na ya kwamba Yeye amekuja kutuokoa, na kutufanya huru, kutoka katika kifo cha milele. Yesu anatutaka sisi tuwe mashahidi wake popote tulipo. Anatutaka sisi tusimame katika umati, na kwa ujasiri tupaze sauti na kusema kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu – na kwamba yeye ana nguvu ya kutuokoa. Na kama sisi, tu wenye dhambi, twaweza kumuita na kumwomba Mungu atuokoe - ameahidi kwamba atafanya hivyo.

--------------------------------